

HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA

MKOA WA SHINYANGA

Simu: 028-2762251 General Line

028-2762259 Direct Line

Fax: 028-2763775

Barua pepe: info@shinyangadc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
S.L.P. 113,
SHINYANGA.
TANZANIA.

Barua zote ziandikwe kwa
Mkurugenzi Mtendaji (W) Shinyanga
Unapojibu tafadhali taja

Kumb. Na. SDC/C.4/7/20

21.01.2019

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

I Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga baada ya kupokea Kibali cha Ajira mbadala chenye Kumb.Na.FA.170/376/01/95 cha tarehe 27.12.2018 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa, nafasi za kazi ya **Mtendaji wa Kijiji Daraja la III** na **Dereva Daraja la II** nafasi hizi ni kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

1.0 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – (Nafasi 1)

A. SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe na cheti cha kuhitimu na kufaulu kidato cha Nne, (IV) au kidato cha (VI)
- ii. Aliyehitimu mafunzo ya Astashada /Cheti katika fani ya Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Homboli Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

B. KAZI ZA KUFANYA/MAJUKUMU:

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Usimamizi wa Utawala Bora katika kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- iv. Katibu wa mikutano na Kamati zote za Halmashauri za Kijiji
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- vi. Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na utekelezaji mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji
- ix. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi
- xi. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo ndogo za kijiji

C. UWAJIBIKAJI:

Atawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga

D. MSHAHARA:

Atalipwa mshahara katika ngazi ya TGS B.

